POPULAR VERSION

# ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025




*Kazi na Utu, Tunasonga Mbele*

Popular Version

# ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025

*Kazi na Utu, Tunasonga Mbele*

# Ujumbe wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

*Mwenyekiti wa CCM na Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2025* →



***Ndugu Watanzania Wenzangu,***

Ninawakaribisha katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Ilani hii ndiyo ahadi ya CCM kwa Watanzania juu ya hatua tutakazochukua katika miaka mitano ijayo ili kuendelea kukuza uchumi na kipato cha wananchi, kuinua hali za maisha ya Watanzania wote, kuimarisha ustawi wa jamii, kulinda amani, usalama na utulivu katika nchi, na kudumisha demokrasia na utawala bora.

Kwa niaba ya CCM na Serikali yake, ninawashukuru sana Watanzania wote kwa imani kubwa mliyotupatia kupitia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 uliotupatia uhalali wa kuunda Serikali. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, na katika kipindi chote cha uongozi wake, CCM imeendelea kusimamia mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Ninawaahidi kuwa tutaendelea na mageuzi haya kwa lengo la kutokomeza umaskini, kuinua hali za maisha ya Watanzania wote na kuinua ustawi wa jamii na Taifa letu. Ninaomba muendelee kuiamini CCM na kuwachagua wagombea wake wote kwa nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Urais wa Zanzibar, Ubunge, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani.

***Ndugu Watanzania Wenzangu,*** Mtakumbuka kuwa tulipoanza utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Taifa letu lilipata msiba mkubwa kufuatia kufariki kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyefariki dunia tarehe 17 Machi 2021. Hayati Dkt. Magufuli alikuwa kiongozi jasiri, imara na mwenye uthubutu, sifa ambazo zilimuwezesha kutekeleza na kufanikisha mambo makubwa ndani ya muda mfupi alioongoza. Tutamkumba daima Dkt. Magufuli kwa mchango wake alioutoa katika maendeleo ya nchi yetu. Ninakushukuruni Watanzania wote kwa jinsi mlivyoniombea na kusimama nami katika kipindi cha majonzi na mpito kufuatia msiba huo. Ninamshukuru Mungu kwa jinsi ambavyo ametuwezesha kutunza amani na umoja wa Taifa letu katika kipindi hicho cha mpito. Ninaendelea kuwaahidi kuwa tutaendelea kusimamia utekelezaji wa yote mema ambayo Dkt. Magufuli aliyaanzisha, na kufanya mengine mengi mapya.

***Ndugu Watanzania Wenzangu,*** Mwaka huu Taifa letu limetengeneza Dira mpya itakayoongoza mipango ya maendeleo ya nchi yetu kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. CCM inaunga mkono matarajio yote yaliyoanishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, na tunaahidi kuyatekeleza kikamilifu. Ilani hii imezingatia kikamilifu maudhui na vipaumbele vilivyobanishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2025-2030), CCM itaisimamia Serikali ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani; kulinda amani usalama na utulivu; na kuimarisha ustawi wa Watanzania kwa kuwawezesha kiuchumi na kufungua fursa zaidi za ajira na biashara.

Maudhui ya Ilani hii yamezingatia maoni na matarajio ya wanachama wa CCM, wananchi na wadau mbalimbali walioshiriki kutoa maoni yao kuhusu mambo ya kuzingatiwa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2025. Kwa niaba ya CCM, ninawashukuru wote walioshiriki kutoa maoni yao, ikiwa ni pamoja na wanachama wa CCM, vijana, wanawake, Baraza la Wazee, vyuo vikuu, wasanii, Chama cha Muziki Tanzania, na Shirikisho la Asasi za Kiraia Tanzania.

Ninakishukuru kwa dhati chama changu CCM, kwa kuniteua kuwa Mgombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumteua Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa mgombea wa kiti cha urais wa Zanzibar. Aidha, ninawashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa kuridhia Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa mgombea mwenza. Ninaamini kwa pamoja tutaimarisha mafanikio tuliyoyapata na kufanya mengi mapya katika kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuzingatia kauli mbiu yetu: ***Kazi na Utu, Tunasonga Mbele!***

***Ndugu Watanzania wenzangu,*** ninaomba kura zenu za NDIYO kwangu binafsi nikiwa Mgombea kwa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa nafasi ya Urais wa Zanzibar, na wagombea wote wa CCM katika nafasi za ubunge, ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, na udiwani.

*Mungu Ibariki Afrika; Mungu Ibariki Tanzania.*
*Kazi na Utu, Tunasonga Mbele!*
***Kidumu Chama Cha Mapinduzi***

**Dkt. Samia Suluhu Hassan**

***Mwenyekiti wa CCM na Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2025***

## Ujumbe wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi

*Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar na Mgombea wa Urais wa Zanzibar, 2025* →



***Ndugu Wananchi Wenzangu,***

Kwa heshima na taadhima, ninatumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa kunichagua kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Nane katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2020. Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa ambao umechangia kupata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitano (2020 – 2025) ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, hususan katika ukuaji wa uchumi, kuimarika kwa huduma za jamii ikiwamo sekta za elimu, afya, maji na ujenzi wa miundombinu. Hali hii imewasukuma wanachama wa CCM kupitia Mkutano Maalumu wa CCM uliofanyika tarehe 18 na 19 Januari, 2025 kupendekeza jina langu kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar, kupitia Chama Cha Mapinduzi.

CCM imeendelea kuhakikisha kuwa Ilani za Uchaguzi Mkuu zinaweka mazingatio maalumu kwa Zanzibar, kwa lengo la kudumisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, na kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya tunu ya kitaifa. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2025 – 2030), CCM itaendelea kuweka mazingira bora na kuwa kinara wa maendeleo kwa kuweka vipaumbele muhimu vya kuinua uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni: kuimarisha mshikamano wa Wazanzibari kwa kudumisha amani na maridhiano; kujenga uchumi imara unaonufaisha kila mwananchi; na kuimarisha upatikanaji wa ajira hususan kwa vijana kwa kuzalisha angalau ajira 350,000 katika sekta rasmi na isiyo rasmi ifikapo mwaka 2030.

***Ndugu Wananchi wenzagu,*** CCM itaweka vipaumbele vya kuimarisha uchumi endelevu, huduma za afya, elimu na maji, miundombinu ya usafiri na usafirishaji na nishati, kuanzisha hifadhi ya Taifa ya chakula na kuongeza uzalishaji wa ndani. CCM itaweka msisitizo maalumu kuwainua wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo nafuu na kushajiisha matumizi ya teknolojia na mafunzo ya umahiri katika uzalishaji sambamba na kusimamia upatikanaji wa masoko. Katika kuimarisha haiba ya miji, CCM itaendelea kuanzisha makaazi bora na kusimamia maendeleo ya miji kwa kutumia teknolojia za kisasa za ujenzi unaozingatia mipango miji na usafi wa mazingira. Aidha, CCM itajikita katika kuanzisha hifadhi ya mafuta ya petroli na dizeli ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati hiyo na kupunguza athari za mabadiliko ya bei. CCM itaimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kukuza sekta za uchumi wa buluu, viwanda, kilimo na huduma, kwa lengo la kuongeza Pato la Taifa na ustawi wa wananchi.

Ninakishukuru kwa dhati chama changu, CCM, kwa kututeua; mimi kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais wa Zanzibar, na Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kuridhia Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza. Ninaamini kwa pamoja tutaendeleza mafanikio tuliyoyapata na kufanya mengi mapya katika kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuboresha maisha ya Watanzania.

***Ndugu Wananchi wenzangu,*** Ninaomba kura zenu za NDIYO kwangu binafsi Mgombea wa Urais wa Zanzibar, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wagombea wote wa CCM katika nafasi za Ubunge, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani. ˚

Kwa heshima kubwa, naahidi kwamba, nitaongeza kasi ya maendeleo kwa kuimarisha vyanzo vya mapato, kukuza uchumi wa Zanzibar, na kuhakikisha wananchi wote wananufaika na huduma bora za jamii.

*Mungu Ibariki Afrika; Mungu Ibariki Tanzania.*
*Kazi na Utu, Tunasonga Mbele!*
***Kidumu Chama Cha Mapinduzi***

**Dkt. Hussein Ali Mwinyi**

***Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Mgombea Urais wa Zanzibar***

SURA

# 01.

# *Dira na Msingi wa Mafanikio ya CCM*

## DIRA YA CCM

Kuona Tanzania yenye ustawi kwa wote, nchi inayozingatia na kuheshimu utu, haki na usawa, na Taifa imara linalojitegemea.

## MALENGO YA CCM

1. Kuimarisha Uchumi
2. Kuwawezesha wananchi kuongeza kipato
3. kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii
4. Kuimarisha Miundombinu ya Kisasa ya Usafiri na Usafirishaji
5. Kulinda na kuimarisha amani, utulivu na usalama wa nchi

# 1. Kuimarisha Uchumi

Kukuza Uchumi

TZS



## Mfumuko wa Bei



*Kupungua Wastani wa Mfumuko wa bei*




## Kuongeza Miradi ya uwekezaji



*Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)*




## Kuongezeka kwa Pato la Mwanachi



*Ongezeko la Pato la mtu kwa thamani ya Dola*



# 2. Kuwaweza Wananchi Kiuchumi



Mikopo isiyo na Riba

TZS **99.5** bilioni

*thamani ya mkopo kwa wanawake*

TZS **45.1** bilioni

*thamani ya mkopo kwa wenye ulemavu*

TZS **96.3** bilioni

*thamani ya mkopo kwa vijana*

## Ajira



**Idadi ya Ajira rasmi na zisizo rasmi zilizozalishwa kwa ujumla**




## Masoko



**33**

Idadi ya Masoko yaliyojengwa

## Stendi ya Mabasi




**34**

Idadi ya Stendi za Mabasi zilizojengwa

# 3. Sekta ya Uzalishaji

## Kilimo cha Umwagiliaji



2020

561,383 → 983,466

2024

*Kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji*



## Utoshelevu wa Chakula



*Utoshelevu na usalama wa chakula umeongezeka*

2020

114% → 128%

2024

## Matumizi ya Mbolea



*Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kwa wakulima nchini*




## Mauzo ya Nyama



*Kuongezeka kwa mauzo ya nyama nje ya nchi*




## Mikopo




**280**

*Idadi ya boti za kisasa za uvuvi zilizotolewa kwa Mkopo*

**507**

*Idadi ya vizimba vya ufugaji samaki vilivyotolewa kwa mkopo*

## Umeme



2020: **1,602** megawati → 2024: **3,078** megawati

*Kiwango cha Uzalishaji wa Umeme kimeongezeka kutoka 2020 hadi 2024*

## Umeme Vijijini



***Kuongezeka kwa vijiji vinavyopata huduma ya umeme***



## Idadi ya Watalii



*Idadi ya Watalii kutoka nje ya nchi imeongezeka*

| 2020 | 2024 |
|---|---|
| 620,867 | 5,360,247 |

## Kipato kutokana na Utalii




*Kuongezeka kwa Mapato yaliyotokana na sekta ya utalii*

2020: TZS 700 milioni

2024: TZS 4.0 bilioni

## Sekta ya Madini






## Masoko ya Madini



# 4. Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii.

## Elimu



*Idadi ya Shule za Msingi*




*Idadi ya Shule za Sekondari*




*Kuanza kutolewa kwa mikopo kwa levo za stashahada*

Idadi ya Wanufaika Mkopo



*Idadi ya Wanufaika wa mkopo kwa Wanafunzi wa elimu ya juu*




Bajeti ya Mikopo Elimu ya juu



*Kuongezeka kwa bajeti ya mikopo ya elimu ya juu*




Ujenzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi







*Idadi ya Vyuo vya elimu na ufundi VETA vilivyojengwa*

Ongezeko la Mkopo



*Kuongezeka kwa pesa ya mkopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu*



## Vifo vya Uzazi




*Idadi ya Vifo vitokanavyo na uzazi*




## Vituo vya Afya




*Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya*




## Upatikanaji Dawa na Vifaa Tiba





## Maji









## Mradi wa Maji



# 5. Kuimarisha Miundombinu ya Kisasa ya Usafiri na Usafirishaji

Treni





| 17 | 89 | 1,430 | 10 | 80 |
|---|---|---|---|---|
| idadi ya vichwa vipya vya treni ya umeme | idadi ya mabehewa ya abiria | idadi ya mabehewa ya mizigo | idadi ya treni mpya za mchongoko | idadi ya mabehewa mapya ya abiria |

## Barabara






## Madaraja






## Ndege







## Kituo cha Mafunzo ya Marubani






# 6. Sekta ya Mawasiliano

Huduma za Mawasiliano






*kiwango cha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano ya simu za viganjani*




*kiwango cha usajili wa laini za simu*

Intaneti




*Wateja waliosajili matumizi ya intaneti*

**74%**






# 7. Michezo

Viwanja vya Mpira



***Nchi imefuzu kuwa mwenyeji na mshiriki wa mashindano ya CHAN 2025 na AFCON 2027 ambapo maandalizi yameanza kwa ukarabati na ujenzi wa viwanja vya michezo na mazoezi***

# 1. Kuimarisha Uchumi

Uchumi wa Nchi



*Kiwango cha ukuaji wa uchumi*

| Mwaka | Asilimia |
| --- | --- |
| 2021 | 5.1% |
| 2024 | 7.5% |

# 2. Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

Uchumi wa Wananchi



### Mikopo

**TZS 852 bilioni**

*Thamani ya mikopo iliyotolewa na Wakala wa Uwezeshaji kwa Wilaya 11 za Zanzibar*

**TZS 28 bilioni**

*Thamani ya mikopo iliyotolewa na serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)*

### Ajira kwa Vijana

**78%**

*Ajira kupitia sekta rasmi na isiyo rasmi ndani na nje ya nchi*

# 3. Sekta ya Uzalishaji

Uchumi wa Buluu



*Uzalishaji wa zao la Mwani*



## Eneo la Umwagiliaji



*Eneo lililowekewa miundombinu ya mwagiliaji*




## Utalii



*Idadi ya Watalii*




## Nishati






**72%**

Huduma ya umeme imeunganishwa katika vijiji 222

## Mafuta na Gesi




**1,518**

*Uwezo wa Bohari ya kuhifadhia Mafuta na Gesi (LPG)*

# 4. Miundombinu ya Kiuchumi

## Barabara



*Urefu wa Barabara zilizojengwa Unguja na Pemba*

**376.8** kilomita

### Ujenzi wa Bandari



- Bandari ya Malindi
- Bandari Kavu Maruhubi
- Bandari ya Fumba
- Bandari ya Mkoani Pemba

### Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege (AAKIA)



### Masoko




**3**

*Idadi ya Masoko Makubwa yaliyojengwa Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini*

# 5. Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii

## Elimu








*kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi (kidato cha nne)*




*kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi (kidato cha sita)*

## Afya



**10**

*Idadi ya Hospitali za kisasa za Wilaya zilizojengwa*

## Hospitali




## Maji






**88.22%**
Shehia zote zinazopokea huduma ya maji safi na salama





*Ukarabati wa Kiwanja cha Mpira Amani pamoja na Ujenzi wa kituo cha mafunzo ya mpira kwa vijana Suluhu Academy, Kizimkazi*

SURA

# 02.

# *Ahadi na Maelekezo ya CCM 2025-2030*

## LENGO KUU LA ILANI YA CCM

Kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi.

## MAFANIKIO YA CCM

1. Kuchochea mapinduzi ya uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa kuongeza thamani rasilimali zinazozalishwa nchini;
2. Kuongeza fursa za ajira kwa vijana, kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini;
3. Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii;
4. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji;
5. Kukuza na kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kiuchumi na kijamii;
6. Kudumisha demokrasia na utawala bora;
7. Kuendelea kudumisha amani, utulivu na usalama
8. Kudumisha utamaduni wa taifa, na kukuza sanaa na michezo.

# A. Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa, Fungamanishi, Jumuishi na Shindani

## Kuimarisha ukuaji jumuishi wa uchumi

Kuimarisha ukuaji jumuishi wa uchumi: kukuza uchumi kwa wastani kwa mwaka








## Kuimarisha sekta binafsi

Kuanzisha Mfuko Maalum wa kuwezesha upatikanaji wa mitaji, hususan wajasiriamali wa biashara ndogo, za kati, na kampuni changa

# Sekta za kimageuzi za uzalishaji





## Miundombinu ya Umwagiliaji

Kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji




## Kuongeza Tija katika Kilimo

Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora na kwa bei nafuu na kutoa ruzuku ya pembejeo

## Vituo vya Ukodishaji Zana za Kilimo

Kuanzisha vituo vya ukodishaji zana za kilimo pamoja na kununua na kusambaza zana za kilimo

**10,000**

***Idadi ya Matrekta yatakayotolewa kwa mkopo***



## Kuimarisha Ufugaji na Uvuvi wa Kisasa

Kutenga, kupima na kumilikisha kwa wafugaji maeneo ya shughuli za ufugaji kutoka ekari **3,466,111 (2025)** kwenda **ekari 6,000,000 (2030)**




## Mitaji na Mikopo

Kuwezesha upatikanaji wa mitaji/mikopo na vifaa kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji, vyama vya ushirika na wawekezaji



## Kuimarisha Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda

Kuendeleza Viwanda saba (07) vya (National Steel, Nachingwea Cashew nuts, Mafuta Ilulu, TPL Mbeya, TPL Shinyanga, Sawmill na Mwanza Tannery)





## Sekta ya Uzalishaji Viwandani

Kuongeza Sekta ya uzalishaji viwandani kufikia **asilimia 9** kwa mwaka kufikia 2030




*Kiwango cha Uzalishaji viwandani kufikia 2030*



## Kuendelea Kuikuza Sekta ya Madini

Kufanya utafiti zaidi wa maeneo yenye madini na kuongeza eneo lililopimwa, ili Kukuza sekta ya madini kutoka **16% mwaka 2025** hadi kufikia **50% mwaka 2030**



## Wachimbaji Madini

Kutenga maeneo maalum ya wachimbaji wadogo wa madini, kuwapatia leseni na kuwaendeleza



## Kuimarisha Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda

Kuifanya Tanzania kuwa kituo cha uuzaji wa madini katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati pamoja na kuimarisha masoko ya madini na vito ikiwemo Tanzanite kwa kujenga jengo la Tanzanite Exchange Centre (TEC) katika eneo la Mirerani, Wilayani Simanjiro



## Kuimarisha Upatikanaji wa Umeme

Kukamilisha usambazaji wa umeme katika vitongoji vyote nchini



## Uzalishaji Umeme

Kuimarisha uzalishaji wa umeme




## Upatikanaji Umeme

Kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika



## Kuimarisha Matumizi Endelevu ya Ardhi

Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na miji kwa kusajili na kumilikisha hatimiliki



## Maeneo ya Ardhi

Kutenga na kulinda maeneo ya ardhi ya kilimo kwa wakulima na malisho ya mifugo



## Kuimarisha Sekta ya Utalii

Kuimarisha mikakati ya kutangaza na kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi.




*Kiwango cha Idadi ya watalii kwa mwaka kufikia 2030*

## Viwanja vya Ndege

Uboreshaji viwanja vya Ndege katika mbuga za wanyama na maeneo ya utalii ikiwemo Mikumi na Serengeti



# B. Kuongeza fursa za ajira kwa vijana, kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini:



## Ajira kwa Vijana

Kuzalisha idadi ya ajira kwa vijana katika sekta rasmi na isiyo rasmi.

**8.5 milioni**

*Kiwango cha Idadi ya ajira kufikia 2030*

## Vituo vya Uwezeshaji Kiuchumi

Kuanzisha vituo vya uwezeshaji kiuchumi katika mikoa ili kusogeza huduma kwa wananchi na kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF).



# C. Kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii

## Elimu

Kuongeza fursa za elimu kwa kuendelea kutoa elimu bila ada kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari



## Maslahi Walimu

Kupitia upya maslahi ya walimu na kuyaboresha ipasavyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi na nyumba za walimu



## Elimu ya Ufundi

Kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga vyuo vipya vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na polytechnics




**65**

*Vituo vipya vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi*

## Afya

Kuwezesha wananchi wote kujiunga na huduma ya bima ya afya



## Maji

Kuongeza idadi ya kaya zilizofikiwa na huduma za maji safi na salama kwa asilimia isiyopungua **90**

90%

## Mpango wa Taifa wa Maji

Kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji na kuendelea na utekelezaji wa mtandao wa Taifa (National Water Grid) wa kusambaza maji kwa kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo kujenga mradi wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Singida na Dodoma

Kukamilisha mradi wa maji wa miji 28

Kukamilisha mradi wa maji Kiwira - Mbeya

Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa

Mradi wa maji wa Kidunda

Kuchimba visima na mabwawa



## Makazi ya Watu



Kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi ili kuwezesha wananchi hususani wa kipato cha chini kujenga nyumba bora za kisasa na kwa gharama nafuu

## Kuboresha Makazi



Kuendelea kuboresha makazi mijini kwa kuhakikisha makazi, nyumba na majengo yote yanarasimishwa kwa kupimwa, kupangwa, na kumilikishwa

# D. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji

## Barabara na Madaraja



Kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara za makao makuu ya mikoa na wilaya

Kuhakikisha kuwa barabara zote za vijijini zinakarabatiwa na kujengwa, ili ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka

Kuanza ujenzi wa barabara za juu (flyovers) katika makutano ya barabara katika maeneo ya Morocco, Mwenge, Magomeni na Tabata, Jijini Dar es Salaam

Kukamilisha miradi ya ujenzi wa madaraja inayoendelea ikiwemo madaraja ya Malagarasi Chini (Kigoma), Mkenda (Ruvuma), Godegode (Dodoma), Mzinga (Dar es Salaam), Simiyu (Mwanza), Nzali (Dodoma), Ugalla (Kigoma), Sanza (Singida), Mitomoni (Ruvuma), Malagarasi Juu (Kigoma), Mkundi (Morogoro), Pangani (Tanga), Kalebe (Kagera), na Mto Msimbazi eneo la Jangwani (Dar es Salaam)

Ujenzi wa barabara kubwa za kuunganisha mikoa na nchi jirani ikiwemo barabara ya njia nne ya Igawa – Uyole – Songwe – Tunduma (km 218), barabara ya Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 162), barabara ya Tarime – Mugumu (km 87), barabara ya Geita - Bukoli – Kahama (Busoka) km 133.9, barabara ya Mabokweni – Maramba – Bombo Mtoni – Umba hadi Same (278km)

Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya IV - VI katika barabara za Ali Hassan Mwinyi – Morocco - Mwenge - Tegeta na Mandela kuanzia makutano ya Ubungo na Bandari, makutano ya Mandela/ Tabata – Tabata Segerea na Tabata - Kigogo





## Reli

Ujenzi wa reli ya Standard Gauge Mwanza - Isaka (km 341), Makutupora – Tabora (km 368), Tabora - Isaka (km 165), Tabora-Kigoma (506), Uvinza- Musongati (km 156.6)

Kujenga reli na kuweka usafiri wa treni za mijini (Metro) katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma ili kupunguza msongamano na kurahisisha usafiri

Kujenga reli ya kisasa ili kuunganisha Bandari ya Tanga kuelekea Arusha hadi Musoma (km 1,108)



## Bandari

Kujenga bandari mpya ya Bagamoyo

Kuboresha bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Kigoma, Kalema, Musoma na bandari kavu katika eneo la Kurasini - Dar es Salaam, Kwala - Pwani na Ihumwa – Dodoma



### Meli

Kukarabati meli zilizopo katika maziwa makuu na kujenga meli mpya za mizigo na abiria katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi



### Usafiri wa Anga

Kuendelea kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania kwa kununua **ndege nane**

8

*Idadi ya ndege zitakazonunuliwa*




## E. Kukuza Matumizi ya Sayansi na teknolojia

### Sayansi na Teknolojia

Kuandaa na kutekeleza mkakati maalum wa kutumia teknolojia zinazoibukia ikiwemo akili unde, matumizi ya roboti, setilaiti, block chain kuimarisha ufanisi na tija katika uzalishaji na utoaji wa huduma



Kuunda na kurusha Satelaiti za kimkakati katika orbit za anga za juu kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo mawasiliano, ufuatiliaji wa hali ya hewa, na uchunguzi wa sayari

Kuongeza wigo wa wananchi wa vijijini kutumia teknolojia ya habari ili kunufaika na fursa zitokanazo na shughuli za uzalishaji kiuchumi na kijamii



# F. Kudumisha Utamaduni wa Taifa, na Kukuza Sanaa na Michezo

## Utamaduni

Kuongeza jitihada za kuitangaza lugha ya Kiswahili kimataifa

Ujenzi wa Eneo Changamani la Utamaduni



## Sanaa za Maonesho




Kuweka mfumo imara wa kulinda hakimiliki za wasanii kwa kuimarisha sheria za hakimiliki ili kuhakikisha wasanii wananufaika na kazi za sanaa

Kujenga studio za uzalishaji wa filamu zinazotumia teknolojia na vifaa vya kisasa

Kujenga kituo kikubwa cha burudani (arena) kwa ajili ya maonesho ya kazi za Sanaa na burudani nyingine kitaifa na kimataifa

## Michezo



Kuanzisha na kuendeleza shule za michezo (sports academies) kwa lengo la kuandaa wana michezo wa leo na baadaye

Kujenga viwanja vya kisasa vya michezo vyenye viwango vya kimataifa ikiwemo FIFA na Olympic (***AFCON City - Arusha***)





Kawe - Dar es salaam


SGR - Mwanza


AFCON City - Arusha


Metro - Dodoma

SURA

# 03.

# *Mazingatio Maalumu ya Ilani Kuhusu Zanzibar*

## Lengo Kuu la Ilani ya CCM Zanzibar

Kukuza uchumi jumuishi kwa maendeleo endelevu na ustawi wa Wazanzibari wote

## Vipaumbele vya Ilani ya CCM Zanzibar

a. Kuendelea kuwaunganisha Wazanzibari na kudumisha umoja, amani, utulivu, ushirikiano, maridhiano na uvumilivu;

b. Kujenga uchumi imara ambao utazingatia usawa na kunufaisha maeneo yote ya Zanzibar;

c. Kuimarisha upatikanaji wa ajira kwa vijana kwa kuzalisha angalau ajira 350,000 kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi ifikapo mwaka 2030;

d. Kuhakikisha uhakika wa chakula kwa kuanzisha hifadhi ya Taifa ya chakula na kuongeza uzalishaji wa ndani;

e. Kuimarisha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kuendelea kutoa mikopo, kushajihisha matumizi ya teknolojia na mafunzo ya umahiri;

f. Kuanzisha Makaazi bora na upendezeshaji wa miji kwa kuzingatia teknolojia mpya ya ujenzi, mipango miji na mipango ya usafi wa mazingira pamoja na udhibiti wa taka;

g. Kuanzisha hifadhi ya kitaifa ya mafuta (petrol na dizeli) Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mafuta na kupunguza athari za mabadiliko ya bei;

h. Kuweka vivutio maalumu vya kushajihisha uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta kuu za uchumi ikiwemo uchumi wa buluu, viwanda, kilimo, na huduma;

i. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, maji, na umeme; na

j. Kuimarisha hifadhi ya jamii kwa wote.

## Mazingatio Maalumu ya Ilani Kuhusu Zanzibar Maeneo Makuu ya Utekelezaji

a. Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa na Endelevu

b. Kuongeza Fursa za Ajira, Kipato na Kupunguza Umaskini

c. Kuchochea Mapinduzi ya Kidijitali

d. Huduma za Habari na Mawasiliano

e. Kuboresha Maisha ya Watu na Ustawi wa Jamii

f. Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

# A. Kuchochea Mapinduzi ya Uchumi wa Kisasa na Endelevu

## Mfumuko wa Bei

Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuwa chini kwa mwaka.

**5%**

*Kiwango cha mfumuko wa bei kupungua*



## Pato la Taifa




Kuongeza ukuaji wa pato la taifa kwa mwaka

## Fursa za Ajira

Kuzalisha fursa mpya za ajira kwa vijana

**350k**

*Idadi ya Fursa za Ajira*



## Kipato cha Mtanzania

Kuongeza kipato cha Mtanzania kwa Dola za Marekani kwa mwaka



# Sekta za kimageuzi za uzalishaji - Zanzibar

## Kilimo

Uzalishaji wa karafuu na makonyo




## Mifugo

Kutoa mkopo ya ng'ombe wawili kwa vijana kila mkoa kwa kila mwaka

**60**

*Idadi ya vijana watakaopokea mkopo*

## Misitu na Maliasili

Kuwa na Zanzibar ya kijani kwa kupanda miti ya aina mbalimbali

**5 milioni**

*Idadi ya Miti kupandwa*

## Ushirika

Kutoa mafunzo kwa Vyama Vya Ushirika

**2,500**

*Idadi ya Vyama vitavyopokea mafunzo*

## Nishati

Kujenga Bohari ya Gesi yenye ujazo Mkubwa

**tani 1,500**

*Ujazo wa Bohari ya Gesi*



## Biashara

Kuongeza thamani ya Biashara (trade value) kwa Zanzibar






## Viwanda

Kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa






## Ardhi

Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki kwa lengo la kurahisiha upatikanaji wa huduma za ardhi



# Ukuaji wa Uchumi wa Buluu

## Utalii




Uzalishaji wa karafuu na makonyo



## Uvuvi




Kuongeza uzalishaji wa samaki hadi kufikia 2030



## Kilimo cha Mwani




Kuongeza uzalishaji wa zao la mwani




## Mafuta na Gesi Asilia

Kuendeleza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia

Kujenga kituo cha kudumu cha kuhifadhi taarifa na sampuli za mafuta na gesi asili eneo la Fumba.

## Bandari

Kuendelea na ujenzi wa bandari jumuishi katika maeneo ya Mangapwani

## Usafiri wa Baharini

Kuanzisha usafiri wa teksi za baharini kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kwa wananchi na watalii

## Usimamizi wa Bahari

Kuweka Miongozo na Mipango endelevu ya Matumizi ya Bahari (Marine Spatial Plan)

Kuimarisha ulinzi na usalama wa watumiaji wa bahari na mali zao



## Uhifadhi na Urithi wa Kale

Kuandaa mpango maalum wa uhifadhi na kuendeleza urithi wa asili, majengo ya kihistoria na tamaduni za Zanzibar

**15%**

*Asilimia ya Hifadhi za Mali za Urithi wa kihistoria*



# B. Kuongeza Fursa za Ajira, Kipato na Kupunguza Umaskini

## Wahitimu

Kuendeleza programu za kujenga umahiri kwa wahitimu




## Fursa za Ajira

Kulinda fursa za ajira kwa vijana wazawa na kuwajengea uwezo wa kuajirika

## Sekta Binafsi

Kuandaa programu za kuwavutia wawekezaji na sekta binafsi ili kuajiri vijana

## Ajira Mpya

Kuanzisha ajira mpya kwa wananchi wa Zanzibar hasa vijana katika sekta rasmi na zisizo rasmi Unguja na Pemba

**350,000** *Idadi ya Ajira Mpya kwa Vijana*

# C. Kuchochea Mapinduzi ya Kidijitali

## Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Uchumi wa Kidigitali na Ubunifu

### Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia:



Kuendesha mafunzo ya matumizi ya kidigitali katika sekta za sanaa, mitindo, na bidhaa za kitamaduni

Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na matumizi ya teknolojia mpya

### Uchumi wa Kidijitali na Uvumbuzi



Matumizi bora ya teknolojia za kidigitali ili kuongeza ufanisii wa huduma za serikali.

Kupanua matumizi ya maudhui ya kidigitali na bidhaa za kitamaduni ili kuongeza mvuto kwa watalii na kukuza uchumi wa kidigitali.

### Utafiti na Ubunifu



Kuongeza idadi ya watafiti na kuhakikisha matokeo ya tafiti yanatumika katika mipango na maamuzi ya serikali.

Kuhakikisha vyuo vya elimu ya ufundi, kati na juu vinaanzisha vituo atamizi

# D. Huduma za Habari na Mawasiliano

## Kuimarisha Mawasiliano na Upatikanaji wa Habari

### Upatikanaji wa Habari



Kuboresha huduma za vyombo vya habari ili habari ziwafikie wananchi wote

Kuimarisha Tume ya Utangazaji ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.

### Mawasiliano



Kuanzisha mji wa kidigitali (Smart City) katika Fumba na kuiunganisha Zanzibar na mkonga wa kimataifa (International Gateway)

Kuimarisha mfumo wa Serikali Mtandao (e-Governance) ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na kuhakikisha wananchi wote wanapatiwa anuani za makaazi kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi.

# E. Kuboresha Maisha ya Watu na Ustawi wa Jamii

## Malengo Makuu katika Kuboresha Ustawi wa Jamii

### Elimu

Lengo ni kujenga uwezo wa kitaaluma, ufundi, na ujuzi kwa wananchi wa Zanzibar.




### Afya

Lengo ni kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza vifo vinavyotokana na magonjwa yanayozuilika.



### Maji

Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji safi, na salama



### Makundi Maalum

Lengo ni kuhakikisha usawa na haki kwa kila mtu katika jamii, wakiwemo watu weye ulemavu, wanawake na watoto.

## Hifadhi ya Jamii kwa Wote

Lengo ni kupunguza ugumu wa maisha, kuwainua wananchi kiuchumi kupunguza umasikini, kuleta utulivu na ustawi wa jamii.



## Maendeleo ya Mipango Miji, Nyumba na Makazi

Lengo ni kujenga uwezo wa kitaaluma, ufundi, na ujuzi kwa wananchi wa Zanzibar.




## Utamaduni, Sanaa na Michezo

Kuendelea kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Kiswahili, historia, sanaa na utamaduni wa Mzanzibari; Kukamilisha maandalizi ya nchi kuwa mwenyeji wa mashindano ya mpira wa miguu Barani Afrika (AFCON-2027) kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo, kuhamasisha na kuboresha miundombinu wezeshi.



# F. Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

## Malengo Makuu katika kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji

### Usafiri wa Anga na viwanja vya Ndege

Kuongeza idadi ya safari za ndege zinazoingia na kutoka nje kwa mwaka

**125,056**

*Idadi ya Safari za ndege kwa mwaka*

Kuendeleza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Pemba ikiwemo kuongeza urefu wa njia ya kurukia ndege (run way), pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria

**2,500**

*Urefu wa njia ya kurukia ndege*

Kuendeleza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi;

Kujenga uwanja wa ndege wa Paje utakaohudumia ndege ndogo za abiria

**70**

*Idadi ya abiria watakaobebwa na ndege ndogo*






## Usafiri wa Ardhini na Miundombinu ya Barabara

Kujenga barabara ya Tunguu – Makunduchi (km 48), Fumba – Kisauni (km 12), Mkoani – Chake (km 43.5) na Barabara ya Utalii Nungwi (km 12)

Kujenga barabara za ziada (feeder)

**275.9** kilomita

*Umbali wa Barabara za Ziada*

Kuendelea kujenga barabara za mijini

**100.9** kilomita

*Umbali wa Barabara za Mjini*

Kuendelea kujenga barabara za vijijini

**80** kilomita

*Umbali wa Barabara za Vijijini*



KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE